

TANGAZO

Muswada huu utakaowasilishwa Bungeni, umechapishwa kwa taarifa kwa umma pamoja na maelezo ya madhumuni na sababu zake.

Dar es Salaam,
19 Desemba, 2011

PHILLEMONT L. LUHANJO,
Katibu wa Bunge

MUSWADA

kwa

**Ajili ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Mabadiliko
ya Katiba ya mwaka 2011.**

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1. Sheria hii itaitwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011 na itasomwa ikiwa ni sehemu ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka, 2011.

Jina la
Sheria
Na. 8 ya
mwaka
2011

2. Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011 inafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:

Mareke-
bisho ya
Vifungu
vya 6 na
18

(a) katika kifungu 6(5), kwa kufuta katika aya ya (a)-

(i) “mkato”;

(ii) maneno “au kiongozi wa chama cha siasa katika ngazi zote”;

- (b) katika kifungu cha 18, kuongeza masharti yafuatayo mara baada ya kifungu kidogo cha (5):

“(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Tume inaweza kuruhusu asasi, taasisi au makundi ya watu kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa wanachama wake kutoa maoni yao juu ya Rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni hayo kwenye Tume.”

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika vifungu vya 6 na 18 vya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011 kwa sababu mbili, Kwanza kuondoa kizuizi cha kutoteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume baadhi ya watu ambao si Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar au Madiwani. Pili kuruhusu asasi, taasisi au makundi ya watu kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa wanachama wake kutoa maoni yao juu ya Rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni hayo kwenye Tume.

Dar es Salaam,
14 Desemba, 2011

CELINA O. KOMBANI,
Waziri wa Katiba na Sheria